# Watumishi Wa Kristo

**na**

**Ellis P. Forsman**

# Watumishi Wa Kristo

**na**

**Ellis P. Forsman**

**Oktoba 14, 2011**

# Watumishi Wa Kristo

## Gal. 1:10

### Sisi ni watumishi

- Gal. 1:10, "*Maana sasa je ni wanadamu ninaowashawishi, au Mungu? Au nataka kuwapendeza wanadamu? Kama ningekuwa hata sasa nawapendeza wanadamu, singekuwa mtumwa wa Kristo.*"
- Rum. 6:16, "*Hamjui ya kuwa kwake yeye ambaye mnajitoa nafsi zenu kuwa watumwa wake katika kumtii, mmekuwa watumwa wake yule mnayemtii kwamba ni utumishi wa dhambi uletao mauti, au kwamba ni utumishi wa utii uletao utii.*"

### Sisi ni zaidi ya watumishi

Gal. 4:7, "*Kama ni hivyo, wewe si mtumwa tena bali u mwana; na kama u mwana basi u mrithi wa Mungu.*"

## Mtumishi mwema ni nani?

### Mtiifu

- Rum. 6:17-18, "*Lakini Mungu na ashukuriwe kwa maana mlikuwa watumwa wa dhambi, lakini mliitii kwa mioyo yenu ile namna ya elimu ambayo mliwekwa chini yake; na mlipokwisha kuwekwa huru mbali na dhambi, mkawa watumwa wa haki.*"
- 1 Pet. 1:22, "*Mkiisha kujitakasa roho zenu kwa kuitii kweli, hata kuufikilia upendano wa ndugu usio na unafiki, basi jitahidini kupendana kwa moyo.*"

### Kristo mfano wetu

- Fil. 2:5-8, "*Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo Yesu; ambaye yeye mwanzo alikuwa yuna namna ya Mungu, naye hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho; bali alijifanya kuwa hana utukufu akatwaa namna ya mtumwa, akawa ana mfano wa mwanadamu; tena alipoonekana ana umbo kama mwanadamu alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, naam mauti ya msalaba.*"

- Ebr. 5:8-9, "*Na ingawa ni mwana alijifunza kutii kwa mates ohayo yaliyompata; naye alipokwisha kukamilishwa, akawa sababu ya wokovu wa milele kwa watu wote wanaomtii.*"

## Wenye bidii

2 Tim. 2:15, "*Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli.*"

## Si wavivu

- Rum. 12:11, "*Kwa bidii si walegevu; mkiwa na juhudi katika roho zenu; mkimtumikia Bwana.*"
- 2 Pet. 1:5-11, "*Naam, na kwa sababu iyo hiyo mkijitahidi sana kwa upande wenu, katika imani yenu tieni na wema, na katika wema wenu maarifa, na katika maarifa yenu kiasi, na katika kiasi chenu saburi, na katika saburi yenu utauwa, , na katika utauwa wenu upendano wa ndugu, na katika upendano wa ndugu upendo. Maana mambo hayo yakiwa kwenu na kujaa tele, yawafanya ninyi kuwa si wavivu wala si watu wasio na matunda, kwa kumjua Bwana wetu Yesu Kristo. Maana yeye asiyekuwa na hayo ni kipofu hawezi kuona vitu vilivyo mbali amesahau kule kutakaswa dhambi zake za zamani. Kwa hiyo ndugu jitahidini kufanya imara kuitwa kwenu na uteule wenu, maana mkitenda hayo hamtajikwaa kamwe. Maana hivi mtaruzukiwa kwa ukarimu kuingia katika ufalme wa milele wa Bwana wetu mwokozi wetu , katika imani yenu tieni na wema, na katika wema wenu maarifa, na katika maarifa yenu kiasi, na katika kiasi chenu saburi, na katika saburi yenu utauwa, , na katika utauwa wenu upendano wa ndugu, na katika upendano wa ndugu upendo. Maana mambo hayo yakiwa kwenu na kujaa tele, yawafanya ninyi kuwa si wavivu wala si watu wasio na matunda, kwa kumjua Bwana wetu Yesu Kristo. Maana yeye asiyekuwa na hayo ni kipofu hawezi kuona vitu vilivyo mbali amesahau kule kutakaswa dhambi zake za zamani. Kwa hiyo ndugu jitahidini kufanya imara kuitwa kwenu na uteule wenu, maana mkitenda hayo hamtajikwaa kamwe. Maana hivi mtaruzukiwa kwa ukarimu kuingia katika ufalme wa milele wa Bwana wetu mwokozi wetu Yesu Kristo.*"
- Ebr. 4:11, "*Basin a tufanye bidii kuingia katika raha ile, ili kwamba mtu ye yote asije akaanguka kwa mfano uo huo wa kuasi.*"

## Mnyenyekevu, mtiifu; anayetumika

- Mat. 18:4, "*Basi ye yote ajinyenyekeshaye mwenyewe kama motto huyu, huyo ndiye aliyemkuu katika ufalme wa mbinguni.*"
- Mat. 20:26-27, "*Lakini haitakuwa hivyo kwenu; bali mtu ye yote anayetaka kuwa mkubwa kwenu, na awe mtumishi wenu; na mtu ye yote anayetaka kuwa wa kwanza kwenu na awe mtumwa wenu.*"
- Rum. 12:10, "*Kwa pendo la udugu, mpendane ninyi kwa ninyi kwa heshima mkiwatanguliza wenzenu;*"

## Kristo mfano wetu – aliosha miguu ya wanafunzi

- Yoh. 13:5, 14-16, "*Kisha akatia maji katika bakuli, akaanza kuwatawadha wanafunzi miguu na kuifuta kwa kile kitambaa alichojifunga. Basi ikiwa mimi niliye Bwana na mwalimu nimewatawadha miguu imewapasa vivyo kuwatawadha ninyi kwa ninyi. Kwa kuwa nimewapa kielelezo; ili kama mimi nilivyo watendea nanyi mtende vivyo. Amin, amini nawaambia ninyi mtumwa si mkuu kuliko Bwana wake wala mtume si mkuu kuliko yeye aliyempeleka.*"
- (Kuoshwa miguu kulihitajika katika nchi hiyo.)
- Mwanzo 18:4, "*Na yaletwe basi maji kidogo mkanawe miguu mkapumzike chini ya mti huu.*"
- Mwanzo 24:32, "*Na mtu yule akaingia katika nyumba, akawafungua ngamia naye akatoa majani na malisho kwa ngamia, na maji ya kuoshea miguu yake, na miguu ya watu waliokuwa pamoja naye.*"

## Hodari

- Yosh. 1:5-8, "*Hapatakuwa mtu ye yote atakayeweza kusimama mbele yako siku zote za maisha yako; kama nilivyo kuwa pamoja na Musa ndivyo nitakavyokuwa pamoja na wewe; sitakupungukia wala sitakuacha. Uwe hodari na moyo wa ushujaa, maana ni wewe utakayewarithisha watu hawa nchi hii niliyowaapia baba zao ya kwamba nitawapa. Uwe hodari na ushujaa mwingi uangalie kutenda sawasawa na sheria yote aliyokuamuru Musa mtumishi wangu usiiache, kwenda mkono wa kuume au wa kushoto upate kufanikiwa sana kila uendako. Kitabu hiki cha torati kisiondoke kinywani mwako, bali yatafakari maneno yake mchana na usiku,*

*upate kuangalia kutenda sawasawa na maneno yote yaliyoandikwa humo; maana ndipo utakapoifanikisha njia yako, kisha ndipo utakapositawi sana.*"

- Rum. 8:31, "*Basi tuseme nini juu ya hayo? Mungu akiwa upande wetu ni nani aliyejuu yetu?*"

## Anayejitoa kwa bwana wake

Mfano. Kut.21:1-6, "*Basi hukumu utakazoziweka mbele ya watu ni hizi ukimnunua mtumwa wa Kiebrania atakutumikia muda wa miaka sita; mwaka wa saba atatoka kwako huru bure. Kwamba aliingia kwako pekee yake tu, atatoka hivyo pekee yake; kwamba ameoa mkewe atatoka aende pamoja naye. Kwamba ni bwana wake aliyempa huyo mke, naye amemzalia wana wa kiume au wa kike, yule mke na wanawe watakuwa ni mali ya bwana wake, naye mume atatoka pekee yake. Lakini huyo mtumwa akisema wazi wazi, mimi nampenda bwana wangu, na mke wangu na watoto wangu, sitaki mimi kutoka niwe huru; ndipo hapo huyo bwana waake atamleta mbele ya Mungu na kumleta mlangoni; na bwana wake atalitoboa sikio lake kwa uma; ndipo atamtumikia siku zote.*"

**Anayetafuta kutumika tu.** Gal. 1:10, "*Maana sasa je ni wanadamu ninaowashawishi, au Mungu? Au nataka kuwapendeza wanadamu? Kama ningekuwa hata sasa nawapendeza wanadamu, singekuwa mtumwa wa Kristo.*"

**Hawezi kuwatumikia mabwana wawili.** Mat. 6:24, "*Hakuna mtu awezaye kutumikia mabwana wawili; kwa maana atamchukia huyu na kumpenda huyu; ama atashikamana na huyu na kumdharau huyu. Hamwezi kumtumikia Mungu na mali.*"

**Mvumilivu.** Yakobo alitumika miaka 14 ya Raheli. Mwanzo 29:15-30, "*Laban akamwambia Yakobo kwa sababu wewe ni ndugu yangu je! Unitumikie bure? Niambie mshahara wako utakuwa nini? Laban alikuwa na mabinti wawili jina la wa mkubwa ni Lea, na jina la mdogo ni Raheli. Naye Lea macho yake yalikuwa dhaifu, lakini Raheli alikuwa mzuri wa umbo, na mzuri uso. Yakobo akampenda Raheli akasema, nitakutumikia miaka saba kwa kumpata Raheli, binti yako mdogo. Laban akasema afadhali nikupe wewe kuliko mtu mwingine, kaa kwangu. Yakobo akatumika miaka saba kwa kumpata Raheli. Ikawa machoni pake kama siku chache tu kwa vile alivyompenda. Yakobo akamwambia Labani, nipe mke wangu maana siku zangu zimetimia; niingie kwake. Labani akakusanya watu wote wa mahali pale, akafanya karamu. Ikawa wakati wa jioni akamtwaa Lea binti yake, akamletea Yakobo, naye akaingia kwake. Labani akampa Lea mjakazi wake Zilpa, awe mjakazi wake. Ikawa kulipokuwa asubuhi kube! Ni Lea. Akamwambia Labani nini hii uliyonitenda? Sikukutumikia kwa Raheli? Mbona umenidanganya?*

*Labani akasema, havitendeki hivi kwetu, kumtoa mdogo kabla ya mkubwa; timiza siku zake saba nasi tutakupa huyu kwa utumishi utakaonitumikia, miaka saba mingine. Yakobo akafanya hivi, akatimiza siku zake saba. Naye akampa Raheli binti yake kuwa mkewe. Labani akampa binti yake Raheli mjakazi wake Bilha, awe mjakazi wake. Akaingia kwa Raheli naye, akampenda Raheli kuliko Lea, akatumika kwa ajili yake miaka saba mingine.*"

Usichoke kutenda mema. Gal. 6:9, "*Tena tusichoke katika kutenda mema; maana tutavuna kwa wakati wake tusipozimia roh.*"

Vumilia kila mara. Efe. 6:18, "*Kwa sala zote na maombi mkisali kila wakati katika Roho, mkikesha kwa jambo hilo na kudumu katika kuwaombea watakatifu wote;*"

**Mwaminifu kwa bwana wake.** 1 Kor. 4:1-2, "*Mtu na atuhesabu hivi kuwa tu watumishi wa Kristo na mawakili wa siri za Mungu. Hapo tena inayohitajika katika mawakili, ndiyo mtu aonekane kuwa mwaminifu.*"

**Mwaminifu hata kufa.** Ufu. 2:10, "*… uwe mwaminifu hata kufa nami nitakupa taji ya uzima.*"